TAASISI YA KUTHIBITI UBORA WA MBEGU TANZANIA

TOSCI

TANZANIA OFFICIAL SEED CERTIFICATION INSTITUTE

SIMU: +255-23-264 0034
NUKUSHI: +255-23-264 0035
BARUA PEPE: info@tosci.go.tz
WAVUTI: www.tosci.go.tz

MAKAO MAKUU:
S.L.P. 1056
MOROGORO
TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

## KUIDHINISHWA KWA MATUMIZI YA AINA ZA MBEGU ZA ASILI KWA MAZAO MBALIMBALI KWA MWAKA 2024/2025

Kwa kuzingatia mchango wa mbegu za asili katika kulinda nasaba za mimea kwa ajili usalama wa chakula, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 12 (a) na 13 (3) cha Sheria ya Mbegu Sura ya 308, ameidhinisha matumizi ya aina 13 za mbegu za asili za mazao ya mahindi (aina 4), mpunga (aina 4), maharage (aina 2), na papai (aina 3).

Aina hizo za mbegu za asili zimekuwa zikitumiwa na wakulima katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na mbegu hizo kuwa na sifa zinazopendwa na wakulima ikiwemo kukomaa kwa muda mfupi, kuwa na ladha nzuri, kunukia vizuri na kuwa na ukinzani dhidi ya magonjwa ya mimea.

Orodha ya aina za mbegu zilizoidhinishwa na kusajiliwa katika Daftari la Taifa la Orodha ya Aina za Mbegu ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Zao | Aina ya Mbegu | Mhusika |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | Mehhe | Wakulima |
| | | Combas | Wakulima |
| | | Njano | Wakulima |
| | | Erkutoo | Wakulima |
| 2. | Mpunga | Makanyaga | Wakulima |
| | | Mbawambili | TARI |
| | | Lawama | TARI |
| | | Kalamata | TARI |
| 3. | Maharage | Wifi Nyegera | TARI |
| | | Mujunza | TARI |
| 4. | Papai | ASPEC1 | Mkulima (ASPEC) |
| | | ASPEC2 | Mkulima (ASPEC) |
| | | ASPEC3 | Mkulima (ASPEC) |

Hatua hiyo ya usajili wa aina hizo za mbegu inatoa wigo mpana kwa wakulima kuchagua aina za mbegu zinazofaa kwa uzalishaji kulingana na eneo husika, mahitaji ya soko pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kujenga mifumo himilivu ya chakula hapa nchini.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
24 Juni, 2025